Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI**

THE WORLD BANK
IBRD • IDA

Kingdom of the Netherlands

GOBIERNO DE ESPAÑA

# TAARIFA FUPI YA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI


## KATIKA HAFLA FUPI YA UTIAJI SAINI MKATABA WA UJENZI WA MTO MSIMBAZI

20 Aprili, 2026
Ukumbi wa JNICC, Dar es Salaam





# LAYOUT OF FINAL EARTHWORKS OUTCOME



# TAARIFA FUPI YA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI KATIKA HAFLA FUPI YA UTIAJI SAINI MKATABA WA UJENZI WA MTO MSIMBAZI



## 1. UTANGULIZI


Mradi wa Msimbazi una lengo la kukabiliana na mafuriko katika eneo la chini la Bonde la Msimbazi (Jangwani) pamoja na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi kutokana na umuhimu wa eneo husika kwa uchumi wa Dar es Salaam. Mradi unatarajiwa kuhamisha nyumba zaidi ya 3,000 na kupanua na kuongeza kina cha Mto Msimbazi pamoja na kuongeza uwezo wa mawanda ya mafuriko katika eneo la chini la Bonde la Msimazi. Udongo utakaotokana na upanuzi huo utatumika kutengeneza maeneo salama kwa makazi na biashara pembezoni mwa Bonde; jumla ya hekta 57 zinatarajiwa kupatikana kwa matumizi hayo.

Mradi utajenga daraja jipya eneo la Jangwani lenye urefu wa mita 390 na karakana mpya ya mabasi ya mwendokasi katika eneo la Ubungo Maziwa. Vilevile mradi unatarajiwa kuboresha maeneo korofi katika eneo la juu la Bonde pamoja na kuratibu shughuli za kibinadamu ili kudhibiti mmomonyoko wa udongo unaotuama eneo la chini na kusababisha mafuriko. Mradi ulianza rasmi mwezi Februari 2023 na utatekeleza kwa muda wa miaka sita (6).

**3000** nyumba zitakazohamishwa kupisha eneo la Mradi

Jumla ya Hekta **57** kupatikana kwa matumizi ya Mradi

Daraja Jipya lenye urefu wa mita **390** kujengwa eneo la Jangwani




Ramani inayoonesha eneo la utekelezaji wa Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi

## 2. GHARAMA YA MRADI


Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa dola za marekani milioni 260 zinazotokana na mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (dola milioni 200), mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Uhispania (dola milioni 30), na ruzuku kutoka Serikali ya Uholanzi (euro milioni 30).

Ruzuku kutoka Serikali ya Uholanzi itachangia katika utekelezaji wa mkataba wa kupanua na kuongeza kina cha Mto Msimbazi pamoja na kuongeza uwezo wa mawanda ya mafuriko katika eneo la chini la Bonde la Msimazi tu. Kwa mujibu wa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Uholanzi, fedha hizi zitalipwa moja kwa moja kwa mkandarasi baada ya kazi iliyokamilika kuthibitishwa na Serikali. Kwakuwa kazi hii bado ipo kwenye mchakato wa manunuzi, bado ruzuku hii haijaanza kutumika.

# 3. UTEKELEZAJI WA MRADI

## 3.1 Fidia kwa Waathirika wa Mradi

Mpaka sasa mradi umeshalipa kiasi cha Shilingi Bilioni 73.69 kama fidia kwa waathirika wa mradi wapatao 2551 kwa ajili ya kupisha uendelezaji wa eneo la chini la Bonde; kundi hili ni la waathirirka wanaoathirika na mafuriko. Kundi la pili ni la waathirika wapatao 314 watakaoathirika na ujenzi wa matuta kwa ajili ya maeneo salama ya makazi na biashara. Viwango vya fidia kwa kundi la pili vimepelekwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata idhini ya kufanya uthamini.



Mkazi wa Msimbazi Bondeni ndg. Joseph Stephano Selemani akisaini fomu za malipo ya fidia wakati wa zoezi wa uhakiki wa ulipaji wa fidia katika Mradi wa Uboreshaji wa Bonde la Mto Msimbazi.

## 3.2 Ujenzi wa Daraja Jipya la Jangwani

Ujenzi wa Daraja la Jangwani ulianza rasmi mwezi Mei 2025 chini ya usimamizi wa TANROADS. Mkandarasi anayejenga daraja ni **M/s China Communication Construction Company Ltd.** kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 97.1,** na mtaalamu mshauri wa usimamizi ni **Leporogo Specialist Engineers in JV with Afrisa Consulting Ltd and Dong Myeong Engineering Consultants & Architecture** kwa gharama ya zaidi ya shilingi **bilioni 4.57** Mpaka sasa ujenzi umefikia asilimia 34.





## 3.3 Upanuzi wa Mto Msimbazi

Ununuzi wa mkandarasi wa upanuzi wa mto, mawanda ya mafuriko na maeneo salama ya makazi na biashara upo katika hatua za mwisho ambapo leo hii tunashuhudia utiaji Saini mkataba husika. Jumla ya makampuni 11 yaliomba zabuni ya kufanya kazi hii na Kampuni ambayo imepata zabuni hii ni **M/s China Civil Engineering Construction Cooperation in joint venture with China Railway Construction Cooperation Harbour Channel Engineering Bureau Group Co. Ltd.** kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 195.66.**

Lengo kuu la mkataba huu ni kukabiliana na mafuriko kwa kupanua na kuongeza kina cha Mto Msimbazi, kuongeza uwezo wa mawanda ya mafuriko na kujenga maeneo salama (hekta 57) yasiyofikiwa na mafuriko kwa ajili ya makazi na biashara katika eneo la chini la Bonde la Mto Msimbazi. Kimsingi, kazi hii inaenda kuweka msingi wa kazi ya ujenzi, ambayo ni kujenga Bustani ya Jiji na maeneo ya makazi na biashara, ambavyo kwa sasa vipo kwenye hatua ya usanifu. Mkataba huu unajumuisha kazi kuu zifuatazo.

## 3.3 Upanuzi wa Mto Msimbazi

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ubomoaji wa nyumba ambazo zimeshafidiwa na kuhamisha huduma za umeme, maji na simu katika eneo la mradi kwa ajili ya kupisha ujenzi. | **Hekta 420** |
| 2. | Uondoaji wa mimea pamoja na udongo wa juu na madampo yaliyopo eneo la mradi. | **Hekta 270** |
| 3. | Kulinda eneo la mradi kwa kuweka nguzo (beacons) | **900** |
| 4. | Kupanua na kuongeza kina cha Mto Msimbazi na kuongeza uwezo wa mawanda ya mafuriko na kusafirisha udongo uliochimbwa kwenda kwenye maeneo yalikusudiwa kwa ajili ya makazi na biashara. | **Mita za Ujazo 2,330,000** |
| 5. | Kuimarisha kingo za Mto Msimbazi | **Mita 35,100** |
| 6. | Kujenga maeneo ya makazi na biashara kwa kushindilia udongo kwa vimo vilivyosanifiwa. | **Mita za Ujazo 1,560,000** |
| 7. | Kujaza tabaka la udongo salama katika eneo la Bustani ya Jiji na maeneo ya makazi na biashara. | **Mita za Ujazo 660,000** |
| 8. | Kuimarisha kingo za maeneo ya makazi na biashara | **Mita 8,100** |
| 9. | Upandaji wa majani na mimea mbalimbali katika kingo za mto pamoja na maeneo ya makazi na biashara | **Hekta 260** |
| 10. | Ujenzi wa karakana ya usimamizi na utunzaji wa mchanga utakaokuwa unapunguzwa kutoka mtoni kwa ajili ya matumizi ya ujenzi | **2** |

Muda wa utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuwa miezi 24 tangu mkataba utakapotimiza masharti ya kuanza, inakadiriwa kuwa masharti ya kuanza mkataba yatatekelezwa ndani ya miezi miwili (2) kuanzia sasa. Hivyo, mkataba unatarajiwa kuanza rasmi ifikapo mwezi Juni 2026.

## 4. Changamoto

Eneo la mradi kwa sasa lina wafanyabiashara wa usafirishaji wa mizigo, soko la Kigogo na magereji ambao hawana miundombinu ya kudumu lakini wanaendesha biashara zao katika eneo la mradi. Ili mradi uanze, inabidi wafanyabiashara wote hawa kuhamishwa na kupelekwa maeneo mengine kwa ajili ya kuendelea na biashara zao. Tunaiomba Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam kusaidia kutafuta maeneo mbadala ambayo yatawekewa miundombinu ya msingi kwa ajili ya kuwahamisha wafanyabiashara hawa ili kuwawezesha kuanza biashara zao.



## HABARI PICHA





After during flood events





